BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Kumi – Tarehe 16 Mei, 2026
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Zitasomwa.

## I. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

116 MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ:

Sheria ya Kudhibiti Vileo, Namba 9 ya mwaka 2020 iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, imeunda Bodi ya Vileo ambayo imepewa majukumu kadhaa. Hata hivyo, imeonekana kuwa Bodi hiyo haifanyi kazi kwa ufanisi uliotarajiwa kama Sheria inavyotaka, kwa kuwa Bodi hiyo hukosa ufanisi wa kutekeleza kazi zake, hasa katika kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, ambapo Sheria inasitisha Leseni za Vileo lakini bado kuna maeneo ya Zanzibar, leseni hizo zinafanyakazi na Bodi haichukui hatua.

(a) Kwa kuwa Bodi hiyo inaonekana kutofanyakazi kwa ufanisi unaotakiwa, kwa mapungufu hayo makubwa, kwanini haivunjwi na kuundwa upya.

(b) Je, ni lini Serikali itaifuta na kuiandika upya Sheria ya Kudhibiti Vileo namba 9/2020, ili pamoja na marekebisho mengine, kuweka muundo mpya wa Bodi itakayokuwa na uhuru, nguvu na uimara katika kusimamia Sheria.

312. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kumeongezeka changamoto ya uchafuzi wa mazingira ya bahari (marine pollution) katika baadhi ya maeneo ya mwambao wa Zanzibar. Hali hii inachangiwa kwa kiasi kikubwa na kutupa taka ngumu kiholela ambapo wakati wa mvua taka hizi husombwa na maji ya mvua kupitia mitaro ya maji ya mvua (storm water drainage systems) na mikondo ya maji na hatimae kuishia baharini. Jambo hili hupelekea athari kubwa kwenye mifumo ya Ikolojia ya Bahari.

(a) Je, Serikali ina mikakati gani madhubuti ya kuimarisha usimamizi wa taka katika maeneo ya mijini na vijijini, ili kuzuia taka zinazosombwa na maji ya mvua kuingia baharini, kupitia mitaro ya maji ya mvua na mikondo ya maji.

(b) Je, Serikali imeweka hatua gani za kudhibiti utupaji holela wa taka katika maeneo ya fukwe, ili kulinda mazingira ya mwambao na kuimarisha hadhi ya Zanzibar kama kitovu cha utalii wa bahari.

(c) Ni mikakati ipi ya kisheria na kiutendaji iliyowekwa na Serikali katika kudhibiti utupaji wa taka baharini unaofanywa na baadhi ya wasafiri wa vyombo vya majini pamoja na wavuvi.

## Wizara ya Kazi na Uwekezaji

465. MHESHIMIWA JUMA HASSAN THABIT (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Uwekezaji:

Licha ya jitihada mbalimbali zinazofanyika za kufungua fursa za ajira kwa wazanzibari, bado kuna baadhi ya wawekezaji wanakiuka misingi ya kiutumishi kwa waajiriwa wao.

(a) Je, ni waajiri wangapi wameshtakiwa kutokana na uvunjifu wa haki na stahiki za wafanyakazi wao.

(b) Je, ni kigezo gani kinatumika kumpa kipaumbele mzanzibari katika ajira binafsi.

**Wizara ya Fedha na Mipango:**

457. MHESHIMIWA JUMA HASSAN THABIT (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Mapigano yanayoendelea nchini Irani kwa kiasi kikubwa yatapelekea athari ya kiuchumi kwa kupanda gharama za maisha ndani ya taifa letu.

Je, Serikali imejipanga vipi katika kukabiliana na kupanda gharama za maisha kwa wananchi wake.

476. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Ili kuendana na viwango vya Kimataifa vya Uhasibu wa Sekta ya Umma, Serikali ya Zanzibar inaendelea na maandalizi ya kuhamia katika mfumo wa kihasibu wa *Accrual Basis* kutoka *Cash Basis.*

(a) Je, mabadiliko haya yamepokelewa vipi na wadau mbalimbali.

(b) Katika kuelekea kwenye mabadiliko hayo, je, Serikali inakabiliwa na changamoto gani.

(c) Je, Serikali imeweka mikakati gani kuhakikisha kwamba mabadiliko haya yanafanikiwa kwa ufanisi mkubwa.

**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:**

20. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Bandari ya Shumba Mjini inatarajiwa kuanza kutumika hivi karibuni, hali itakayorahisisha shughuli za kuingia na kutoka bandarini hapo.

Je, ni lini Serikali itaweka kivuko cha kisasa katika Liko la Kwawari Shumba Mjini.

54. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Jimbo la Ole) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Hivi karibuni Serikali ilitoa tamko la kubadilisha mfumo wa usajili wa vyombo vya moto na vibati vya nambari (Plate number) kwa vyombo vya maringi mawili na magari hapa Zanzibar.

(a) Je, ni sababu gani iliyopelekea Serikali kufanya mabadiliko haya kwa vyombo vya moto.

(b) Je, kwa takwimu ni vyombo vingapi vinatakiwa kubadilishwa kwenda kwenye mfumo mpya na fedha kiasi gani Serikali itazipata.

**<u>Wizara ya Maji, Nishati na Madini:</u>**

112. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Hivi karibuni Serikali ilitutangazia kuwa kuna meli ya kuzalisha umeme mbayo awali ilikuwepo nchini Kenya na sasa imeletwa Zanzibar kwa ajili hiyo. Kuna taarifa kuwa Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO), tayari limeshafikisha njia (line) kwa ajili ya kupokea umeme huo katika eneo la Mtoni Zanzibar. Hata hivyo, inaonekana meli hiyo bado haijaunganisha njia hiyo.

(a) Kwa nini mpaka hivi sasa umeme huo haujaunganishwa kutoka kwenye meli hiyo na kuingizwa kwenye "line' ambayo ZECO wameshaweka tayari.

(b) Je, Serikali imejiridhisha vipi kama meli hiyo ina uwezo wa kuzalisha umeme huo.

(c) Na endapo itabainika kuwa meli hiyo haina uwezo, hatua gani zitafuata kurejesha gharama za kuileta.

**<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>**

298. MHESHIMIWA MOHAMMED ALI SALIM (Jimbo la Ziwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa kuna mabadiliko mapya na maboresho ya mitaala ambayo inaenda kubadilisha mfumo wetu wa elimu.

(a) Je, Serikali ya Zanzibar imepeleka walimu wetu wangapi kwenda kujifunza katika nchi za nje zenye mitaala ya ufundi inayofanana na mageuzi ya mitaala yetu ili kuendana na mabadiliko ya dunia yenye tija.

(b) Ni walimu wangapi hadi sasa waliofundishwa kwa vitendo kutoka mfumo wa sasa kwenda katika matumizi ya vifaa vya mchipuo mpya kama wa uvuvi na kilimo ili kuwajenga kuwa na ufanisi uliokusudiwa.

392. MHESHIMIWA DKT. NASRA NASSOR OMAR (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Wanafunzi wanaosoma Elimu Mjumuishi (Inclusive Education) wanakabiliwa na changamoto ya vifaa muhimu vya kujifunzia.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia Wanafunzi wa Elimu Mjumuishi vifaa muhimu vya kujifunzia ili wapate elimu stahiki.

(b) Kwa kuwa hivi sasa kuna changamoto ya vifaa hivyo, ni ipi hali halisi ya upatikanaji na utumiaji wa vifaa vya kufunzia kwa wanafunzi wanaoendelea na masomo ya Elimu Mjumuishi kwa mwaka huu wa masomo.

(c) Kwa kukosekana vifaa vya kujifunzia kwa wakati, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha malengo ya kuanzishwa kwa elimu hiyo yanatimia.

**Wizara ya Afya:**

448. MHESHIMIWA JUMA HASSAN THABIT (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa Hospitali ya Kibondeni inapokea idadi kubwa ya wagonjwa tofauti wa ndani na nje ya jimbo la Fuoni. Na kwa kuwa kuna ukosefu wa baadhi ya vitendea kazi katika hospitali hiyo na vyengine vimeharibika.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha huduma na vitendea kazi vikiwemo, kuharibika kwa *"Change Over Switch"* ya Generata; Ukosefu wa mitungi ya gesi wakati wa kusafirisha wagonjwa kwenda Hospitali za Wilaya; Ukosefu wa Gari ya Kuchukulia Wagonjwa (Ambulance); Ukosefu wa Chumba Maalum cha Faragha cha Kujifungulia Wazazi na Ukosefu wa ghala maalumu (store) la kuhifadhia madawa.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

127. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Hivi karibuni Mahakama ya Zanzibar ilitoa uamuzi wa kulipwa fidia wafanyabiashara waliofungua kesi ya kupigwa na baadhi ya Askari wa Mamlaka ya Mji Mkongwe, ambapo Wizara inadaiwa kuwa tayari kuwalipa. Hata hivyo, mpaka hivi sasa wafanyabiashara hao inadaiwa hawajalipwa fidia hiyo.

(a) Je, kama bado, kwa nini malipo ya fidia hiyo hayajafanyika kwa wafanyabiashara hao.

(b) Je, kwa hukumu hiyo, Wizara imechukuwa hatua gani ili matukio kama hayo yasijitokeze na kusababisha kulipishwa faini kama hizo.

257. MHESHIMIWA KHAMIS MOHAMMED AMRAN (Jimbo la Mkoani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Katika jimbo la Mkoani Pemba, yapo maeneo mengi ya kihistoria ambayo kwa sasa yameanza kupoteza uhalisia wake.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuyahifadhi maeneo hayo pamoja na kuyatumia kwa shughuli za utalii ili kuongeza kipato kwa wananchi wa Mkoani.

## Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

82. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Hivi karibuni kimesikika kilio cha wavuvi wa Wilaya ya Wete kupitia Mwenyekiti wa Kamati za Wavuvi ya Wilaya ya Wete kuhusiana na mfumko wa kodi wanazotozwa wavuvi wa Wilaya ya Wete, pamoja na maeneo mengine. Miongoni mwa kodi hizo ni kiasi cha asilimia ya kodi wanachotozwa wavuvi kutokana na pato wanalopata kwa siku moja ambayo kwa hali za wavuvi wetu wadogo wadogo ni fedha nyingi kulingana na hali ya uvuvi wenyewe.

(a) Je, Serikali imekisikia kilio hiki na kama wamekisikia hatua gani zimeanza kuchukuliwa, ili kuwapa ahuweni wavuvi wa Wilaya ya Wete na maeneo mengine.

(b) Je, kwa kuwa wavuvi wetu bado uvuvi wao ni wa hali ya chini, kwa nini Serikali isiwatoze ada ndogo tu ya usafi badala ya kuchukuwa kiasi cha asilimia katika pato lao la kila siku ambalo huwa ni dogo.

(c) Je, Serikali kupitia Mamlaka zinazohusika hawaoni kwa sasa ni bora wakasitisha kutoza asilimia ya fedha kutoka katika pato la kila siku la wavuvi ili kusaidia wavuvi kuongeza vipato vyao.

**Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji:**

259. MHESHIMIWA KHAMIS MOHAMMED AMRAN (Jimbo la Mkoani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Ajira na Uwezeshaji:

Serikali ina mikakati gani ya kukabiliana na ongezeko la ukosefu wa ajira kwa vijana hapa Zanzibar.

## II. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2026/2027.

**Zanzibar,**
**16 Mei, 2026.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA**
**WAWAKILISHI, ZANZIBAR**